

UJUMBE WA SIKU YA UKIMWI DUNIANI TAREHE 1 DESEMBA 2007

Kwa Wanashirika la Yesu wa Afrika na Madagaska

Makala haya yameandaliva na Fr. Fratern Massawe S.J. Msimamizi wa Shirika la Yesu Afrika na Madagaska

Wapendwa maswahiba katika Kristo,

Siku ya UKIMWI duniani, 2007, ni wakati stahiki wa kukumbushana wajibu wetu tuliopewa na Mungu, tukiendelea kuitikia changamoto muhimu za nyakati zetu. Kwa kuzisoma dalili za Virusi vya Ukimwi na Ugonjwa wa Ukimwi, tunatambua kuwa hizi ni nyakati za kuonyesha fadhila ya upendo na huruma ya Kimungu kwa wale wote wanaoteseka na wanaohitaji msaada.

Dhamira kuu ya Siku ya Ukimwi Duniani na ya Mapambano dhidi ya Ukimwi kimataifa kwa miaka ijayo ni **UONGOZI** wenye wito: “**Kuwa mstari wa mbele. Zuia Ukimwi. Timiza ahadi!**” Kwa miaka ya hivi karibuni AJAN, Mtandao ulioanzishwa na Wakuu wa Shirika la Yesu wa Afrika na Madagaska (JESAM) mnamo mwaka 2002, imekuwa ikitusaidia katika kuitikia wito wetu. Wakati AJAN inaadhimisha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake, imekuwa mstari wa mbele siyo tu katika utume wa Kanisa na kuzuia kuenea kwa maradhi ya Ukimwi Barani Afrika, bali pia kuwapa matumaini Wakristo ili wabaki thabiti katika kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi.

Ni dhahiri AJAN imepata mafanikio makubwa tangu kuasisiwa kwake, mathalani tovuti, machapisho mbalimbali yanayosomwa na hadhira kubwa, uhusiano mzuri wa AJAN na mashirika yasiyo ya kiserikali, makazi ya AJAN Kangemi, Nairobi, yaliyo na hazina kubwa ya elimu ya Ukimwi—na mengine mengi japokuwa si dhahiri, lakini yana umuhimu wa pekee. Mafanikio mengine yamejidhihirisha katika malezi na mafunzo yanayotolewa miongoni mwa Wanashirika wa Yesu wanaofanya utume wa Ukimwi. Kimsingi, mafunzo na malezi yamewawezesha wanashirika kujiona kuwa wao pia ni sehemu ya waathirika wa ugonjwa wa Ukimwi; na jambo la kutia moyo idadi ya Wanashirika wanaofanya utume imekuwa ikiongezeka kwa kiasi kikubwa.

Tunapaswa kukumbuka kuwa AJAN itafanikiwa iwapo sisi sote tutafanya kazi kwa ushirikiano. Kwa hiyo jukumu kuu la AJAN ni mosi, kuwatia moyo Wanashirika la Yesu wa Afrika na Madagaska ili wawe mstari wa mbele katika kupambana na Virusi vya Ukimwi na Ugonjwa wa Ukimwi; pili, kuwa pamoja na wanaume, wanawake na watoto ambao tayari wameshaambukizwa maradhi ya Ukimwi na wale watakoathirika na maradhi haya; tatu, kushirikiana na waathirika katika kutetea haki zao na wakati mwingine kupigania haki hizo kwa niaba yao na kusaidia kuanzisha elimu juu ya athari za Ukimwi itakayokuwa kinga kwa watu na jumuiya kwa jumla. Mwisho, kuendeleza mtazamo wa kiteolojia na wa elimu ya jamii ambao ndiyo mhimili wa juhudi.

Katika mapambano dhidi ya Ukimwi tunahitaji sana nguvu ya uongozi. Uongozi ambao unavuka mipaka ya kawaida ya utendaji na hivyo kutoa huduma bila ya hofu inayosababishwa na unyanyapaa au ufahamu mdogo wa maradhi ya Ukimwi. Aidha, uongozi maana yake ni kujihusisha na mambo anuwai yanayohusiana na Virusi na Ugonjwa wa Ukimwi na vile vile kuwa mdadisi na mwakilishi hodari wa kichungaji. Hatimaye, uongozi ni ujasiri wa imani yetu na uaminifu yakini katika mapambano magumu na ya muda mrefu dhidi ya maradhi ya Ukimwi.

Siku ya Ukimwi Duniani inakwenda sambamba na siku ya mwanamke jasiri wa Kikongo ambaye alionyesha sifa za kiongozi asiye na hofu. Mwenye Heri Anuarite Nengapeta, alikuwa ni mkunga na mtawa wa familia takatifu. Mwanamke huyu kijana ambaye aliyatoa maisha yake kwa kuwahudumia watu mbalimbali, aliuawa 1964 baada ya kukataa kutimiza matakwa ya kiongozi wa waasi nchini Kongo, ya kumtaka afanye naye mapenzi. AJAN inaungana na vijana wengi wa Kiafrika kumwenzi na kumwona Anuarite kama mfano wa uaminifu na usafi wa mwili ambaye anatia matumaini, uvumilivu na kujiamini katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Kama leo hii mwenye heri Anuarite angelikuwa hai, yumkini angelikuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya Ukimwi. Hata hivyo tunaamini huko alipo anayoyatenda

ni zaidi ya vita tulivyonavyo. Ndiyo maana tunasema, kwa kuungana naye, pamoja watakatifu na wahenga wetu bado tuna nafasi nzuri ya kushinda vita dhidi ya Ukimwi.

Basi tunapoadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani, tuungane pamoja katika kutimiza wajibu wetu wa kuboresha maisha yetu ambayo mara kwa mara yamekuwa yakifupishwa na Virusi vya Ukimwi na maradhi ya Ukimwi. Ni wakati mzuri wa kutathmini huduma zetu katika jamii, nyenzo zetu za uangalizi na aina nyingine za utume, na vile vile kubuni mbinu mbadala za kuelimishana na kuimarisha uwezo wa uchaguzi wa maisha ili kuidhirisha huruma ya Mungu kwa ndugu zetu wanaotuzunguka, hususani wenye kuguswa na janga la Ukimwi.

Fratern Masawe, S.J.

Moderator of

Jesuit Superiors of Africa and Madagascar (JESAM)